Katika Jina La Yesu Kristo

Na

J.D. Logan

(In The Name Of Jesus Christ)

Katika Jina La Yesu Kristo

na

J.D. Logan

Novemba 5, 2011

Katika Jina La Yesu Kristo

"*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38).

Inaonekana kulikuwa na mabadiliko katika kanisa iliyojaribu kuleta sherehe ya kimaandiko ya ubatizo katika kutokuwa na upendeleo na kubadilisha jambo katika sehemu yake.

Hii imekuwa ikiongelewa na kipeperushi kidogo chenye kichwa cha habari, "Biblia Inavunja Toleo na Vipeperushi", iliyoandikwa Jan 5, 2000.

Katika hali fulani, jukumu langu ni kukataa yote yanayokubaliana na ukengeufu wa maandiko. Hataivyo, mwandishi anaonyesha, "Tunatarajia kusikia kutoka kwako…" kama kanisa. Pia, "…kanisa (mwandishi wa kusanyiko) ameandika nyaraka kwa makanisa mengi ya Kristo kupitia taifa hili kuhusu tatizo…"

Zaidi, "…tumesababisha mkanganyiko mwingi miongoni mwa wahubiri wa injili…" naweza kuamini kwa ahakika kwamba hili ni kweli!! Hii imesababisha kuporomoka kwa nyaraka. Niruhusu niongeze katika hilo poromoko!

Dhana

Kulingana na kipeperushi, mwandishi amefikia hitimisho kwamba kubatizwa "*kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu*" siyo ubatizo unaofanyika katika Pentekoste na Petro pamoja na mitume wengine.

Inazidi kuwekwa kwamba ni lazima tubatizwe katika jina la Yesu Kristo (tu) ili ubatizwe kikamilifu.

Nimewahi kusikia kauli hizi kablwa, lakini siyo kutoka kwa mtu anayesema kuwa "Mhubiri wa injili". Kimsingi hii ni sawa na wale wanaofundisha kwamba kuna mtu mmoja pekee katika "utatu mtakatifu, ambaye ni Yesu Kristo" na kwamba "wote wanatakiwa kubatizwa katika jina la Yesu Kristo pekee".

Hataivyo, hakuna ukweli wa kimaandiko kwa mmoja kuliko ilivyo kwa wengine. Wote wako katika makosa!!

Nikinukuu kutoka katika kipeperushi kinachoongelewa, "tunajifunza miaka kadhaa nyuma kwamba kauli kama 'katika jina inamanisha kwa mamlaka ya' iliwekwa pale na mwanadamu ili kujiona wako sawa katika kukataa jina la Yesu Kristo na kujipa usawa kwa maneno ya Mat. 28:19 kama ubatizo ambao ungessamehe dhambi na kuzidisha nafsi katika kanisa."

Hii hudhani kwamba neno lililonukuliwa siyo sawa. Nitaweka, na kuthibitisha kwa maandiko, kwamba “katika jina la’ inaleta maana ya kweli “kwa mamlaka ya”. Hii ni kanuni sahihi ya Biblia na imetumika sehemu nyingi waandishi wa kimitume.

Kauli hii hudhani kwamba sisi tunaofundisha ubatizo kulingana na Mat. 28:19-20 (Agizo Kuu) tumelikataa “jina la Kristo”.

Zaidi katika kinyume, tutaonyesha kwamba hii ndio sherehe sahii ya ubatizo na iliagizwa na Kristo, mwenyewe.

Inakuaje sasa, ubatizo kwa njia hiyo isababishe ‘kukataliwa kwa jina la Yesu Kristo”? Wazo kama hili linaniacha!

Agizo Kuu

kiini cha mkanganyiko ni kile tunachokiita “Agizo Kuu” katika Kristo ukijua kwamba amemaliza kusudi lake duniani na karibuni ni lazima aende kwa Baba yake mbinguni, akawaagizo mitume wake kufanya kitu kipya kabisa.

Mwanzoni Kristo alikuwa amewapa mitume wake maagizo yenye mipaka (kwa Waisraeli pekee), lakini sasa akawaagiza “*Enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeaamini atahukumiwa.*” (Mat. 16:15-16).

Katika Mat. 28:18-20, tunapata mwendelezo wa agizo ili hili kwa matumizi tofauti ya maneno. “*...Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*”

Kwa wakati huu, itakuwa vyema kuangalia uiano wa Mathayo na Marko hasa katika agizo.

Mathayo. “*Enendeni…mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.*”

Marko. “*Nendeni ulimwenguni kote …aaminiye na kubatizwa ataokoka…*”

Tunapaswa kujua kwamba Yesu alikuwa anaandaa agizo jipya kwa mitume. Ilikuwa ni kwa ajili ya “*ulimwengu wote*”, na waliagizwa kuwabatiza wote waliowafundisha. Angalia sherehe iliyoanzishwa na Yesu: “*Kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.*”

Angalia, pia, kwamba waliagizwa kuwafundisha “*...kushika yote niliyowaamuru.*”

Kristo ameagiza kwa jina la "*Baba …Mwana …Roho Mtakatifu.*" Inafuatia kwamba sote tunapaswa kufanya vivyo hivyo. Kufikiria tofauti ni ni kusema mitume walishindwa kutimiza agizo la Kristo. Je huu ndio ushindani wa mwandishi wa kipeperushi chetu?

Njia pekee la hitimisho hili ni kuridhika kwamba Mat. 28:19-20 haipo katika maandiko! Nafikiri mwandishi hatachukua nafasi hii! Hataivyo, Mat. 28:19-20 itabaki kumuumiza.

Tatizo La Mwandishi

Nimechunguza kwa bidii ndani ya kipeperushi na sikuweza kupata majibu ya matatizo yafuatayo yaliyoundwa kwa dhana ya mwandishi.

Kama ubatizo kulingana na Mat. 28:19 ilikuwa si kwa ajili ya msamaha wa dhambi au kumzidisha mtu katika kanisa, kusudi la ubatizo huu ilikuwa nini? Ni kizazi kipi ambacho Yesu kilikuwa katika mawazo ya Yesu alipoliagiza? Na ukomo waa kizazi hiki ilikuwa ni upi?

Ebu ndoga niulize swali tofauti. Ubatizo wa Mat. 28:19 ulikuwa wa Yohana Mbatizaji? Kana siyo, je ulikuwa ni ubatizo wa Yesu? Na kama vyote sawa, ni kwa nini, na ni kwa mamlaka ya nani mitume walifanya ubatizo huu?

Kipengele cha Wakati – Muhimu

Kuna kipengele cha wakati ambao ni muhimu katika ujuzi wa mwandishi wa kipeperushi. Tafadhali angalia:

Tatizo linaegemea katika agizo lililotolewa na Bwana wetu kwa mitume katika Agizo Kuu.

- *Enendeni*.
- "*…mkawafanye mataifa yote*" au "*…hubiri injili kwa kila kiumbe…*"

Ugumu unaingia pale mtu anapochunguza mtiririko wa matukio kati ya usulubisho/ ufufuo/ kupaa na Pentekoste na kuanzishwa kwa kanisa. Anagalia mtiririko huu:

Usulubisho ulitokea katika kilele cha Pasaka, siku 50 kabla ya Pentekoste (Mat. 15:42).

Kristo alijionyesha kwa mitume wake akiwa hai, na akawafundisha kwa siku 40 zilizofuatana (Mdo. 1:1-9).

Ni wazzi kwamba hii iliendelea wakati wa kupaa kwake (Mdo. 1:9-10).

Hii iliacha siku 10 ghafla ili usulubisho utimie. Hatuna hesabu ya kila siku ya siku 10 kufuatia usulubisho, lakini tunaambiwa mambo tofauti iliyotokea. Inawezekana sehemu ya siku 10 ambazo hazikuhesabiwa kikamilifu ilitokea kufuatia ufufuo kabla ya Pentekoste. Ilikuwa ni

wakaati huu ambapo mitume walirudi Yerusalemu (Mdo. 1:20) kutoka Galilaya (Mat. 28:10). Ilikuwa ni wakati huu ambapo mbadala wa Yuda aliteuliwa (Mdo. 1:20-26).

Rekodi iko wazi kwamba ile ya siku 50 kati ya Pasaka na Pentekoste, tuna hesabu nzuri ya matukio ya Yesu na mitume wake. Matukio haya yalijumuisha Yesu kuwafundisha mitume wake biaashara inayohusiana na ufalme wa Mungu (Mdo. 1:3).

Ni wazi kwa mtu yeyote kuwa na akili ambayo haija komaa ya hesabu kwamba kulikuwa haakuna wakati kabisa kwa mitume kutii agizo la "*enendeni ulimwenguni kote, mkawabatize…*" kwa wakati huu. Lini sasa, mitume walipotimiza agizo la Bwana? Je inawezekanaje kwamba mwandishi wa kipeperushi anafahamu kitu ambacho hakikufunuliwa na maaandiko?

Ni salama kusema kwa ujasiri kwamba mitume hawakufundisha wakati huu wa siku 50; walikuwa wanafundishwa na Yesu.

Ugumu unaofuatia kwa mwandishi unakuja kwa wakati huu. Kwa nini Yesu awaagize mitume kufanya yote haya ("*endeni…mkawafundishe…mkawabatize kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu*"), akifahamu kwamba baada ya siku 50 watapewa agizo mpya kubatiza kwa njia nyingine na kwa kusudi tofauti; akijua pia kwamba amewapa agizo ambalo lilikuwa haliwezekani kulitimiza?

Ni ajabu kabisa kwamba mtu anatazama hali isiyowezekana iliyotengenezwa na dhana hii ya ajabu. Lakini kuna zaidi.

Baadhi ya Maswali

Katika kutazama mabishano yote yalitolewa na mwandishi wa kipeperushi hiki, maswali kadhaa yalinitokea ambayo sikupata jibu. Nitayatoa hapa nikitaraji mwandishi atatusaidia kuyajibu. Mtazamo umetolewa katikaa ubatizo wa Mat. 28:19-20.

- Kama ubatizo huu haukuwa kwa ajili ya msamaha wa dhambi au kumweka mtu ndani ya Kristo, kusudi la ubatizo huu ilikuwa ni nini?
- Ni kizazi kipi aambacho ubatizo ulitokea?
- Hii ilikuwa ni kwa muda gani "kizazi"?
- Je ubatizo huu ulikuwa wa Yohana Mbatizaji?
- Je ubatizo huu ulikuwa wa Yesu?
- Kama haukuwa ule wa Yohana au Yesu, ubatizo huu uliagizwa kwa mamlaka ya nani?

Maswali haya yanafaa kujibiwa. Namhitaji mwandishi kuyajibu.

Binafsi sioni suluhisho la tatizo la mwandishi. Kwa makusudi naa dhana yote, ameondoa "Agizo Kuu" ya Mat. 28:19-20, akifanya neno la Yesu kutokuwa na umuhimu bila kujali ukweli kwamba hapa ndiyo sehemu ya kwanza ambayo Yesu alizungumzia wokovu kwa "*ulimwengu wote*."

Tunaongelea agizo hili kama “kuu” kwa sababu moja muhimu sana. ILIKUWWA NI MARA YA KWANZA NA AGIZO PEKEE AMBALO LILIKUSUDIWA KWA ULIMWENGU WOTE, AMBAYO INGEJUMUISHA KILA KIUMBE, NA IWEPO HADI “*ukamilifu wa dahari*.”

NI CHINI YA AGIZO HILI AMBALO NASI TUNAFANYIA KAZI LEO. NI MAMLAKA YAPI MENGINE AMBAYO TUNAWEZA KUDAI KWAMBA IMEBEBA MANENO YA YESU? (Kol. 3:16).

Agizo kuu (Mat. 28:19) ndiyo kiini cha Injili. Kazi binafsi ya Kristo ulitulizwa katika agizo hili.

Mitume walipata mamlaka yao moja kwa moja katika tukio hili, kama tutaakavyoona.

Ilinenwa Na Bwana

“*Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia; Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe.*” (Heb. 2:1-4).

Mtu anawezaa kuangalia Agano Jipya na kupata tukio moja pekee wakati wa huduma ya Kristo ambapo aliongelea wokovu kwa “mataifa yote” akiweka pamoja na misingi ambayo ingetumika. Hii imeandikwa katika Mat. 28:19-20

Ni katika agizo hili ndio mwandishi wa Waebrania anaongelea pale alipoandika, “*...kwanza ulianza kunenwa na Bwana.*”

Kazi Ya Roho Mtakatifu

Yesu alisema (Yohana 15:26, akiongelea Roho Mtakatifu), “*...atanishuhudia.*” Ni nini ambacho Roho Mtakatifu angemshuhudia Yesu kuhusiana na ubatizo na wokovu? Je haiwezi kuwa maneno ya Mat. 28:19-20?

Yesu aaliendelea kusema kazi ya Roho Mtakatifu katika Yohana 14:26, “*Lakini huyo msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu,* ***ATAWAFUNDISHA YOTE NA KUWAKUMBUSHA YOTE*** *niliyowaambia.*”

Je Yesu hakusema maneno ya Mat. 28:19-20 kwa mitume? Tunafanywa kuamini kwamba Roho Mtakatifu aliwakumbusha mitume maneno haya alipowafundisha “*mambo yote.*” (Yohana 14:26).

Roho Mtakatifu alitumwa KWA JINA LA YESU. Ilikuwa ni kazi yake kuwasababisha mitume wakumbuke maneno hayo.

Ambayo inatuleta katika swali linalofuata kimaantiki. Kama Agizo Kuu lilitolewa na Yesu lakini isifanye kazi chini ya ufalme (kufuatia Pentekoste), ni lini na wapi alipobadilisha agizo lake?

Jibu liko wazi; Yesu hakubadilisha "Agizo Kuu." Inatendaa kazi ipasavyo leo na imekuwa ikifanya kazi toka Pentekoste ile ya kwanza. Ndilo agizo ambalo nasi tunapaswa kufanya kazi chini yake leo.

Jina La Yesu Kristo

Petro alipowaagiza wengi siku ya Pentekoste wabatizwe "*kwa jina la Kristo*", je alikuwa anawaagiza kufanya kitu kingine kuliko kile ambacho Yesu aliwaagiza mitume wafanye na kutenda (Mat. 28:19-20)?

Ni vigumu kuamini kwamba yeyote anaweza kutenda hili, LAKINI HIKI NDICHO MWANDISHI ANASISITIZA!!

Inavutia kujua ambaacho Agano Jipya inafunua kwa kuangalia "*katika jina la Yesu Kristo.*" Ebu tuorodheshe machache.

Miujiza Kwa Jina Hili

Mwanamume zaidi ya miaka arobaini aliponywa wakatika kuingia hekaluni (Mdo. 3:6). Hii ilifanyika "*kwa jina la Yesu Kristo.*" msemo huu uliendelea hadi katika Mdo 4:22. "*katika jina la Yesu Kristo*", imeonyeshwa mara nyingi katika maelezo.

- "*...katika jina la Yesu wa Nazareti simama uende...*" (Mdo. 3:6).
- "*...kwa imani mtu huyu amekuwa na nguvu,…* (Mdo. 3:16).
- "*...kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye mlimsulubisha, ...mtu huyu anasimama hapa aakiwa hai.*" (Mdo. 4:10).
- (Kiongozi na makuhani) "*...aliwaagiza wasiseme chochote wala kufundisha kwa jina la Yesu.*"

Matukio yote yaliyotokea wakati huo yalifanyika katika "*jina la Yesu.*"

Tafadhali angalia Mdo. 4:7, "*Walipowaweka katikati wakawauliza, kwa nguvu gani na kwa jina la nani ninyi mmefanya haya?*"

Ni wazi kwamba mambo haya yote yametokana na kauli moja la Yesu katika tukio la "Agizo Kuu", imeandikwa katika Marko 16:18, "*...watawawekea wagonjwa mikono, nao watapata kupona.*"

Yote haya yanaongelea mmalaka. Kuponya "*katika jina la Yesu"* ni kuponya KWA JINA LAKE.

Vilevile, kubatiza, "*kwa jina la Yesu*" ni kubatiza KWA MAMLAKA YAKE. Kwa nini?

Kwa sababu Yesu aliwaagiza mitume kubatiza. Wapi? Katika Mat. 28:19-20. Hili lilikuwa ni agizo ambalo walikuwa wakilifanyia kazi siku ya Pentekoste.

Mtiririko wote wa maelekezo ya "*katika jina la Yesu*" inatoka kwa jina hili mamlaka. "*KATIKA JINA LA YESU* INAMANISHA, KWA MAMLAKA YA YESU, zaidi sana alikuwa Yesu aliyeagiza mitume wabatize kwanza (Mat. 28:19-20).

Hivyo basi, tunahitimisha kwamba tulipobatizwa "*katika jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu*", tulibatizwa sahihi kulingana na agizo la Yesu. Zaidi sana, tunapofanya ubatizo kwa njia hii, tupo sahihi.

Mamlaka Ya Yesu

Mambo yote yaliyofanywa na mitume katika kuhubiri injili, kubatiza, maonyo zaidi katika maisha ya Ukristo, kuwaponya wagonjwa na vilema, n.k., yalifanyika kwa mamlaka ya Yesu.

Mara kabla ya kutoa "Agizo kuu", Kristo alikuwa na "*uwezo wote*" (mamlaka) mbinguni na duniani. Tafsiri sita tofauti zinasema "uwezo" kama "mamlaka".

Yesu alitoa "Agizo Kuu" kwa nguvu ya madai yake ya "*mamlaka yote*" Mat. 28:18). Hivyo basi, haishangazi kwamba ubatizo unaohitajika na mitume ulikuwa ni ule wa misitari ya 19 na 20, "*kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.*"

Hivyo, tunaona Petro alipozungumzia ubatizo "*katika jina la Yesu Kristo*" alikuwa anatenda chini ya 'Agizo Kuu" la Mat. 28:19.

KUNA UBATIZO MMOJA TU (Efe. 4:4). Ubatizo wa "Agizo Kuu" Mat. 28:19) na ule wa Pentekoste (Mdo. 2:38) ni mmoja na unafanana. Hakuna tofauti.

Mengi zaidi yanaweza kuandikwa, lakini muda na nafasi hazitaruhusu. Hili ni somo muhimu sana. Naamini kwamba mwandishi wa kipeperushi kwa kuzingatia atatumia nafasi hii kujibu maswali hapo juu. Tunasubiri majibu.

Wenu katika Kristo,

John D. Logan.